

unge wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood (wa pili kushoto), akisaidiana na wananchi wa Kata ya Sul-
i, kuchimba msingi wa ujenzi wa zahanati ya kata hiyo, katika spaa ya Morogoro jana. Mbunge huyo alichangia Sh.
ioni 5, pamoja na mifuko ya saruji na mchanga. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

haina riba na inayolenga kuwainua
kiuchumi na kuondokana na utege-
mezi.

Majosho mawili pekee yafanyakazi Mwanga kati ya 16

Godfrey Mushi, MOSHI

TI ya majosho 16 ya kuogesha
fugo yaliyojengwa kwa ghara-
a kubwa na serikali katika Hal-
ashauri ya Wilaya ya Mwanga,
koani Kilimanjaro, mawili pekee
liyo yenye uwezo wa kufanya kazi
yo kwa sasa.

Uchunguzi uliofanywa na Ni-
she katika sekta hiyo na baadaye
ithibitishwa na Ofisa Mifugo na
vuvi wa Wilaya ya Mwanga, Em-
manuel Sindiyo, unaonyesha kuwa
majosho hayo hayawezi kukidhi

mahitaji ya wafugaji.

Kuogesha mifugo kwenye ma-
josho ya umma yaliyojengwa ma-
hususi kwa ajili ya uogeshaji huo,
kuna faida kubwa kwa wafugaji
walio wengi kuogesha ng'ombe au
mifugo yao kila mara bila gharama
kubwa ambazo zingehitajika kwa
ununuzi wa dawa na bomba au
pampu ya kuogesha.

Sindiyo ameeleza: "Ni kweli
halmashauri ina jumla ya majosho
16 na majosho ambayo ni mazima
ni mawili tu. Hata hivyo, kwa
mwaka mpya wa fedha 2019/2020,

halmashauri itatenga bajeti kwa
ajili ya kuboresha majosho, ingawa
kwa sasa siwezi kusema ni kiasi
gani.

"Zoezi hili la kuogesha mifugo ni
endelevu na la lazima. Kila mwa-
nanchi ambaye ni mfugaji ahakik-
ishe kuwa anapeleka mifugo ili
iogeshwe, hii ni kwa mujibu wa
Sheria ya Mifugo ya Mwaka 203."

Changamoto kuhusu uhai wa
majosho hayo inajitokeza, huku
zoezi la lazima la kuogesha mifugo
likiwa limezinduliwa na Kaimu
Mkurugenzi Mtendaji wa Hal-

mashauri hiyo, Ezekiel Mwasum-
bi, katika Kata ya Kileo. Jumla ya
ng'ombe 577 walipatiwa huduma
hiyo ya kuogeshwa.

Aidha, wakati kukiwa na upun-
gufu huo wa majosho yanayofanya
kazi, tayari Halmashauri ya Wilaya
ya Mwanga imetangaza kuwa
gharama za kuogesha ng'ombe
mmoja katika majosho yake itaku-
wa Sh. 600 na Sh. 100 kwa mbuzi
mmoja.

Pamoja na changamoto hiyo,
idara ya mifugo ya wilaya hiyo
imeeleza kwamba baadhi ya

wafugaji pia hukwepa moja kwa
moja gharama za uogeshaji na
kubaki kujiandaa vyema kwa ajili
ya kutibu mifugo yao, mara tu
wanapooona dalili za maradhi kwa
mifugo yao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa
wataalamu wa mifugo, utaratibu
huo si mzuri kwa kuwa mara ny-
ingine huweza kusababisha ku-
tokea kwa vifo vya wanyama kwa
wingi na kwa ghafla kutokana na
gharama za dawa na hata malipo
kwa wataalamu wa mifugo wataka-
otumika kutibu mifugo hiyo.

Nipashe uk 12, tarehe 28/01/2019